# Je, Biblia Ndiyo Mamlaka Pekee Ya Mungu?

Leo katika ulimwengu tunamoishi kuna vitabu vingi vya dini ambavyo watu wanavifuata. Lakini katika vitabu vyote hivyo ni kipi kilichotoka kwa Mungu na kinaongoza kwenda wokovuni leo? Haya ndiyo maswali tutatakayoyatazama katika maandiko ya Mungu na wala si katika mawazo ya wanadamu.

### Je, Biblia Ni Pumzi Ya Mungu?

Katika 2 Tim. 3:15, tunaona kuwa neno la Mungu ni pumzi ya Mungu. Neno hili ambalo Mungu ametupatia kwa njia nyingi limetoka kwa Baba yetu aliye mbinguni. Neno halikuja zamani kwa mapenzi ya wanadamu, bali watu watakatifu wa Mungu waliongozwa na Roho Mtakatifu kuandika kama Mungu alivyotaka. Kitabu hiki kiliandikwa na watu wakuu kama Yeremia, Ezekieli na wenginia ambao pia waliongozwa na Roho. Katika Yer. 36:2, Mungu alimwambia Yeremia aende na gombo lake na aandike maneno yote aliyoambiwa na Mungu. Katika Eze. 1:3, tunaona kuwa mkono wa Mungu ulikuwa juu ya Ezekieli alipoandika neno la Mungu. Katika Mdo. 1:16, muda mfupi kabla ya Pentekoste tunaona kuwa Mungu alisema na kuandika kupitia kwa Daudi kuhusu unabii wa Kristo. Katika 2 Pet. 1:21, Petro anatangaza kuwaMungu aliwaongoza watu kwa Roho Mtakatifu na kwa hiyo waliandika kama Mungu alivyotaka. Yohana mwenye ufunuo alisema jambo lile lile alipoadika kitabu cha mwisho cha Biblia katika Ufu. 14:13. Yohana alisikia Sauti kutoka mbingni ikisema ANDIKA. Kwa hiyo bila shaka tunaweza kuona kuwa neno la Mungu ni pumzi ya Mungu na liliandikwa kwa ajili yetu leo.

### Je, Biblia Ina Mambo Yote Tunayoyahitaji?

Leo katika ulimwengu tunamoishi, tunaweza kuona kuwa Biblia ni kitabu maalufu kuliko vyote katika Sayari hii. Kinauzwa kila mahali kuliko kitabu cho chote kilichoandikwa na itaendelea hivyo kwa miaka mingi ijayo. Lakini hata hivyo Mungu alikivuvia kitabu hiki na alikituma kupitia mikono ya waandishi 40 kwa kipindi zaidi ya miaka 1600. Mwanadamu leo hawezi kuwa na kitabu kama hicho (yaani hawezi kuandika kitabu kama hicho). Kwa hiyo wanadamu wameanza kuongeaza na kubidilisha neno la Mungu ili kukamilisha yale wayapendayo. Leo madhehebu yana (wana) vitabu vya miongozo kama, Katekesimu na vitabu vingine vilivyoandikwa na watu kupitia watu wenyewe ili wengine wavifuate. Madhehebu mengi leo yanafundisha mambo machache sana kutoka katika Biblia na wameunda vitabu vyao wenyewe vinavyothaminiwa zaidi na kwa hiyo wanavifuata hivyo vilivyoandikwa na watu wala sio Mungu.

Madehhebu hukaa chini katika mabaraza na kuandika vitabu vyao vya miongozo ili wafanye watakavyo. Lakini Mungu hajawahi kumpa mtu mamlaka ya kufanya kitu kama hicho; kwa sababu Biblia ina mambo yote tunayohitaji ili tupate wokovu. Tukiongeza lo lote katika kitabu hicho hatutamfurahisha Mungu. 2 Tim. 3:15-17, kama tulivyoona, maandiko yalimwongoza Timotheo kuutafuta wokovu. Katika 2 Pet. 1:3, Mungu ametupa mambo yote yatupasayo uzima na utauwa. Hapa Petro, ambaye alikuwa na funguo za ufalme anasema Mungu ametupa mambo yote. Katika kitabu cha yuda aya ya 3 mwandishi anaandika kwamba tuishindanie imani ambayo ilitolewa kwa watakatifu

mara moja kwa ajili ya wote.  Neno lilitolewa mara moja kwa watakatifu kwa ajili ya wote.  Sasa kwa nini tunahitaji tena kitu kingine?  Hatupaswi kufanya hivyo.  Maana kama neno la Mungu linavyoonekana katika 1 Pet. 1:25, ni la milele.  Kama wanadamu, wanyama na mimea vinakufa, lakini neno la Mungu litaishi bila kubadhilika milele.

Yesu alisema katika Yn. 8:32, kwamba mtaifahamu kweli na hiyo kweli itawaweka huru. Katika Yn. 17:17, mwandishi anaendelea kusema “Neno lako ndiyo kweli.”  Kama tunaona kuwa tunaweza kuifahamu kweli na neno la Mungu ndiyo kweli, sasa ni kitu gani kinachoongoza kwenda mbinguni?  Kwa kweli ni neno la Mungu katika Mt. 28:18, Yesu anasema, “Nimepewa mamlaka yote wanaotaka kuokolewa watafuata maneno ya Mungu, na Mungu peke yake katika Yn. 12:48, “Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu anaye amhukumuye, neno langu hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.  Maneno hayo yanapatikana ndani ya Biblia, kwa sababu ndani ya Biblia Mungu anazungumza nasi kwa njia ya mwanawe siku hizi za mwisho, Ebr. 1:1-3.

**Namna Gani Kuhusu Vitabu Vya Wanadamu?**

Tayari tumekwishaona kuhusu jinsi kitabu cha Mungu kinavyookoa.  Sasa vipi kuhusu vitabu vingine, vitabu vya mwongozo kama katekesimu, je, vinaokoa leo?

Kwanza ni lazima tufahamu kuwa vitabu vyote vilivyoandikwa na wanadamu, vikaundwa na wanadamu basi vimeandikwa na kuundwa na wenye dhambi kama wewe na mimi. Katika Rum 3:10, “Hakuna mwenye haki hata mmoja.”  Kwa hiyo ina maana watu wote walioishi hapa duniani na wamefikia umri wa kujua mema na mabaya wametenda dhambi.  Sasa kwa nini sisi leo tufuate katekesimu kitabu cha mwongozo cha watu wenye dhambi kama sisi?  Katika 1 Kor. 2:5, Paulo aliandika kuwa, “imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.”  Katika Yer. 17:5 na 7 nabii aliandika, “Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu....Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, ambaye Bwana ni tumaini lake.”  Sisi kama watu leo tusimtegemee mwanadamu, bali Mungu.  Tulitegemee neno la Mungu ambalo linaokoa leo na linatupilia mbali hekima ya wanadamu.  Maana hekima ya wanadamu haiokoi na haiwezi kuokoa.

**Ni Nani Anaweza Kuitafsiri Biblia?**

Leo watu wengi wanafundisha kwamba ni watu fulani tu wanaoweza kujifunza Biblia na wana uwezo wa kutafsiri yaliyoandikwa humo.  Lakini katika 2 Pet. 1:20 neno la Mungu linasema, Mkijua neno hili kwanza, kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kutafsiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.”  Haijalishi wewe ni nani, au mtu ana cheo gani alichopewa na wanadamu.  Hakuna mtu mwenye haki ya kutafsiri neno la Mungu kwa njia anayoitaka yeye.  Neno la Mungu ni jepesi, mtu ye yote anaweza kulisoma na kulifuata kama lilivyoandikwa.  Usitake watu wengine wafikirie na kusoma kwa ajili yako. Inakupasa kufanya mwenyewe.  Sisi kama wanadamu, wote tuna akili sana sawa sawa na mtu mwingine awaye yote bila kujali anarangi gani au ni wa taifa gani.  Wote tunaweza kuufikia ufahamu wa Yesu kwa kufuata neno la Mungu peke yake.  Katika 2 Tim. 2:15, Paulo alimwambia Timotheo ayashike maandiko na aligawe neno la kweli kwa haki.  Kwa maana inawezekana kuligawa neno pasipo haki.  Katika Mdo. 17:10-12, tunaona kuwa Waberoya walikuwa waungwana kuliko wengine.  Waberoya daima walikuwa watu wa kawaida kama wewe na mimi na walisifiwa kwa kusoma maandiko

kama yalivyoandikwa.  Sasa je, ni nani anayeweza kuitafsiri Biblia?  Hakuna, Bali wote tunaweza kusoma na kuona ujumbe rahisi tulipewa sisi sote.  Sio mgumu, ni kiasi cha kuchukua Biblia na kusoma, kuifuata na kupata uzima kwa njia ya neno la Mungu.

**Unatakiwa Kumfuata Nani, Mwanadamu au Mungu?**

Tayari tulikwisha kuona kuwa tusifuate hekima ya wanadamu (1 Kor. 2:5; Yer. 17:5 na 7).  Kwa maana hekima ya wanadamu ni ya bure.  Katika Mt. 15:1-9 tunaona kwa urahisi kwamba tusifuate mapokeo (yanayochukua nafasi ya neno la Mungu) ya wanadamu.  Tukifanya hivyo ibada yetu itakuwa ya bure.
Kama watu wanavyofundisha leo kwamba ni lazima uwaendee watu weingine ili kujifunza neno wanakosea.  Watu wanapofundisha kwamba ni lazima upate maandishi meginie zaidi ya Biblia wanakosea.  Tumekwishaona kuwa hakuna tafsiri ya maandiko ya mtu binafsi katika 2 Pet. 1:20-21.  Vile vile kama tulivyoona kuwa neno la Mungu linatupa mambo yote yanayotuongoza katika uzima na utauwa.  Tumeshaona katika 2 Pet. 1:3, Mungu tayari ameshatupatia mambo yote.  Sasa tunahitaji nini tena?  Kama Mungu anasema, “Nimewapa mambo yote” na wanadamu wanasema, “Tunahitaji Katekesimu hii, vitabu vya miongozo,” n.k. ni nani anayetuambia uongo hapo?

Kwa kila mtu mwenye akili ya kutosha kusoma kipande hiki cha karatasi, basi ana akili za kuweza kuitafuta mbingu kupitia neno la Mungu.  Chukua Biblia, fungua Biblia, nunua Biblia isome, ifuate na uitii.  Usidanganyee na wanadamu ambao wanadhani wana akili kuliko wewe wakidai kuwa maandiko hayawezi kutupeleka wokovuni leo. Kwa maana Mungu alisema, “Nimewapa vitu vyote.”

**Asante,**
**Heath Stapleton**

**www.kanisalakristo.com**
**www.kountzeheath.vox.com**